

Mteja mpendwa wa World Relief WNY,

Tunaelewa kuwa huu ni wakati mgumu unapojitahidi kujenga upya maisha yako nchini Marekani. Tunataka kukuarifu kuhusu mabadiliko ya hivi majuzi yanayoathiri programu zinazo kusaidia. Shirika la World relief inafanya kazi na serikali ya Marekani kutoa ufadhili kwa huduma muhimu, lakini kutokana na mabadiliko kutoka serikalini, rasilimali hizi zimesimamishwa. Matokeo yake, misaada ya kifedha na huduma zingine zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa. Hii ni changamoto mashirika yote ya wale wanaowahamisha wakimbizi, na tunatambua jinsi jambo hili linavyoweza kuwa gumu kwako. Licha ya matatizo hayo, dhamira yetu ya kukuunga mkono ingali imara. Tukiongozwa na imani na misheni yetu ya kujaliana, tutafanya tuwezavyo kukuunganisha na rasilimali zilizopo na watu wa kujitolea ambao wanaweza kusaidia kwa mahitaji maalum.

Ingawa uwezo wetu ni mdogo, kwa sasa tunaweza kutoa usaidizi wa dharura, ikijumuisha:

- Usaidizi wa usafiri kwa miadi muhimu
- Mwongozo juu ya karatasi za DHS (msaada wa umma, SNAP,...)
- Msaada kwa maswali ya bima ya afya
- Msaada wa chakula cha dharura
- Marejeleo ya jumuiya

Ikiwa una maswali au unahitaji usaidizi:

- **Maswali ya Jumla au Wateja wa Makazi Mapya ya Wakimbizi:** Tuma SMS kwa James kwa 585-204-7284 au barua pepe jreid@wr.org
- **Wateja wa Kiukreni (Msaada wa Haraka):** Tuma SMS kwa Svitlana kwa 585-333-6987 au barua pepe strukhlinska@wr.org
- **Wateja wanaozungumza Kiswahili au Kinyarwanda (Msaada wa Haraka):** Tuma SMS kwa Sandra kwa 585-405-1070 au barua pepe suwiringiyimana@wr.org
- **Wateja wanaozungumza Kihispania:** Mtumie Angie Matiz kwa barua pepe adelgado@wr.org

Kwa maelezo ya kisasa katika lugha nyingi, tafadhali tembelea Kituo cha Wateja kwenye tovuti yetu katika worldrelief.org/western-ny/client-hub.

Tunashukuru kwa subira na uthabiti wako na tutaendelea kuwa pamoja nawe unapopitia mabadiliko haya.

Salamu,

World Relief Western NY